Uhuru Jumamosi Julai 19 2025 pg 5

# Madereva 42 wafungiwa leseni

**Na MWANDISHI WETU,**
*Mbeya*

MADEREVA 42 wamefungiwa leseni zao za udereva, baada ya kubainika kukiuka sheria za usalama barabarani na kusababisha ajali mkoani Mbeya.

Madereva hao wamefungiwa leseni katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Juni, mwaka huu.

Akizungumzia baada ya kufanya ukaguzi wa mabasi ya abiria kabla ya kuanza safari kayika Stendi Kuu ya jiji la Mbeya, jana, Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Naibu Kamishna wa Polisi (DCP), Fraisser Kashai kutoka Kamisheni ya Operesheni na Mafunzo, alitoa wito kwa madereva wa mabasi ya abiria kuheshimu na kutii sheria za usalama barabarani kwa lengo la kuepuka ajali.

Kashai aliwataka madereva hao kutii sheria za usalama barabarani na kusisitiza dereva atakayebainika anakiuka sheria za usalama barabarani, jeshi hilo halitasita kumchukulia hatua za kisheria.

Naye, Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani, mkoani Mbeya, Mrakibu Mwandamizi wa Polisi, Notker Kilewa, alisema madereva hao walifungiwa leseni kuanzia Januari hadi Juni, mwaka huu, kutokana na makosa mbalimbali.

Kilewa alieleza jeshi hilo linaendelea kuwachukulia hatua za kisheria madereva wanaoendelea kukiuka sheria za usalama barabarani.

Naye, Ofisa Mfawidhi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Mkoa wa Mbeya, Shaban Mdende alisema mabasi ya abiria yamefungwa kifaa maalumu cha mwenendo kufuatilia mwendo wa vyombo hivyo vya usafiri.

"LATRA na Jeshi la Polisi tunafanya kazi kwa ushirikiano na kufuatilia mwenendo wa mabasi kupitia mfumo wa VTS, ambapo kati ya madereva 42 waliofungiwa leseni, 26 walibainika kupitia mfumo huo," alisema.

Ukaguzi uliofanywa na Naibu Kamishna wa Polisi, Kashai umehusisha ukaguzi wa magari, leseni za udereva, kupima kilevi madereva na utoaji wa elimu ya usalama barabarani kwa abiria.

Lengo la ukaguzi huo ni kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa maelekezo yanayotolewa na kutoa elimu kwa madereva na abiria kuzuia na kudhibiti ajali za barabarani.

CS CamScanner

Habari leo Jumamosi Julai 19 2025 pg 17

# Madereva wa malori waomba Jeshi la Polisi liwabaini wanaotoa vyeti, leseni feki

**Na Eva Sindika**

CHAMA cha Madereva wa Malori ya Masafa Marefu (MDAG) kimeliomba Jeshi la Polisi nchini kutoa taarifa ya watu waliowabaini kutoa vyeti na leseni feki kwa madereva.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi Dar es Salaam, Katibu wa chama hicho, Selemani Mkondo alisema kuna baadhi ya madereva wamekamatwa na jeshi la polisi wakidaiwa wana leseni na vyeti feki wakati nyaraka hizo wamepewa na jeshi hilo.

"Tunaomba kitengo cha usalama barabarani watuambie hivi vyeti feki na leseni feki zinatolewa na nani hapa Tanzania kwa sababu tunavyofahamu sisi tuna mamlaka mbili zinazoshirikiana katika utoaji wa leseni ambazo ni Jeshi la Polisi kitengo cha usalama barabarani na Mamlaka ya Mapato nchini (TRA)," alieleza.

Alihoji kama mamlaka zinazotakiwa kutoa leseni na vyeti ni mbili je hizo leseni na vyeti feki zilizokamatwa zimetoka wapi?

"Leseni nyingi walizozikamata kwa madereva wetu zimetolewa na askari wa jeshi hilo na kila dereva aliyekamatwa alihojiwa na kutoa maelezo wapi alipopata leseni na vyeti walivyovikamata. Sisi tunaomba tuambiwe huu mtandao unaotoa leseni feki ndani ya jeshi hilo unatoka wapi na hatua zilizochukuliwa dhidi ya wahusika," alisema Mkondo.

Aliwaomba viongozi wa jeshi hilo kuangalia namna ya kuwarejeshea leseni madereva waliochukuliwa leseni zinazosemekana feki ili waendelee na kazi ya kutafuta kipato kinachowasaidia wao na familia zao.

"Mtu amechimba mihogo, analima, anaomba msaada kwa ndugu zake ili apate leseni imsaidie katika maisha yake, lakini anajikuta anaangukia pua kwa kupata leseni feki," alisema.

Mkondo aliiomba serikali kuwasaidia madereva kupata mikataba ya uhakika kwa sababu suala hilo limekuwa changamoto kubwa kwao.

"Tuna changamoto nyingi pia, tunaiomba serikali isimamie upatikanaji wa mikataba kwa sababu madereva wengi hawana mikataba wala hawana bima ya afya," alisema.

Alieleza kuwa madereva wanataka ajira zao zipitie kwenye chama cha madereva, ikiwemo kuongezewa mishahara kulingana na ajira zao na uwepo usalama katika maeneo yao ya kazi ambayo ni hatarishi.

Kwa upande wake, Mkuu wa Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, William Mkonda akijibu tuhuma hizo alisema atazungumza na viongozi wa madereva ili kujadili na kuona namna ya kutatua tatizo hilo.

"Unafahamu kuna vyama vingi vya madereva hapa nchini, ninaomba unisaidie pia kuwasiliana na kiongozi wa chama hicho cha madereva waliolalamika afike ofisini tuzungumze kujua namna ya kutatua changamoto hiyo," alisema Kamanda Mkonda.

CamScanner

Habari leo Jumamosi Julai 19.2025 pg 17

# Madereva 42 Mbeya wafungiwa leseni ukiukaji sheria

Na Shukuru Mgoba, Mbeya

MADEREVA 42 mkoani Mbeya wamefungiwa leseni za udereva katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Juni mwaka huu kutokana na makosa ya ukikukwaji wa sheria za usalama barabarani.

Hayo yalibainishwa kwenye taarifa hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Mbeya, Notker Kilewa wakati wa ukaguzi wa mabasi ya abiria kabla ya kuanza safari katika stendi kuu jijini Mbeya.

Kilewa alitaja baadhi ya makosa hatarishi yaliyosababisha madereva hao kufungiwa leseni kuwa ni pamoja na mwendo kasi, kuyapita magari mengine katika maeneo yasiyoruhusiwa pamoja na kuendesha wakiwa wamelewa.

Alitoa wito kwa madereva wote kutii sheria na kanuni za usalama barabarani na kusisitiza kuwa jeshi la polisi halitasita kuchukua hatua kali kwa dereva yeyote atakayebainika kuvunja sheria.

Kwa upande wake, Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani kutoka Kamisheni ya Oparesheni na Mafunzo, Fraisser Kashai aliwahimiza madereva wa mabasi ya abiria kuzingatia sheria za usalama barabarani ili kuepuka ajali na kulinda maisha ya wananchi.

Aliongeza kuwa polisi wataendelea kuchukua hatua kali dhidi ya madereva wote watakaokaidi maelekezo ya kisheria hasa wale wanaojihusisha na makosa hatarishi yanayosababisha ajali.

Naye Ofisa Mfawidhi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Mkoa wa Mbeya, Shaban Mdende alisema mabasi yote ya abiria yamefungwa kifaa maalumu cha mwenendo wa magari (VTS) ambavyo Latra na Jeshi la Polisi hufanya ufuatiliaji wa mwenendo wa mabasi kwa usahihi na ufanisi.

Alieleza kuwa kati ya madereva 42 waliofungiwa leseni, 26 walibainika kutumia mfumo huo, ambao huonesha taarifa za uhalisia kuhusu mwenendo wa magari barabarani.

Ukaguzi uliosimamiwa na Kashai ulihusisha ukaguzi wa magari, leseni za udereva, upimaji wa kilevi kwa madereva pamoja na utoaji wa elimu ya usalama barabarani kwa abiria.

Lengo kuu la ukaguzi huo ni kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya usalama barabarani na kutoa elimu kwa madereva na abiria ili kusaidia kudhibiti na kuzuia ajali.

CamScanner